**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA MLIMBA**

# MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 25-10-2021 KATIKA UKUMBI WA CLUSTER MCHOMBE

**MAHUDHURIO:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Innocent S. Mwangasa | Diwani Kata ya Igima | Mwenyekiti |
| 2. | Eng. Stephano B. Kaliwa | Mkurugenzi Mtendaji (W) | Katibu |
| 3. | Mhe. Farida H. Madege | Diwani Viti Maalumu Mlimba | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Hassan A. Kidapa | Diwani Kata ya Ching`anda | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Emael R. Ndangalasi | Diwani Kata ya Uchindile | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Nestory P. Kyelula | Diwani Kata ya Mbingu | Mjumbe |

**WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Godwin Kunambi | Mbunge Jimbo la Mlimba |
| 2. | Mhe Asha Y. Shomary | Diwani kata ya Chita |

**WAKUU WA IDARA/VITENGO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Awadhi Mashombo | Kaimu Afisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji |
| 2. | Joseph Mgana | Afisa Maliasili (W) |
| 3. | Wakili Nakua, F.A | Mwanasheria (W) |
| 4. | Zaituni Rashid | Kaimu Afisa Utumishi (W) |
| 5. | Witness Kimoleta | Afisa Elimu Msingi (W) |
| 6. | Islam Mposso | Afisa Habari |
| 7. | Suleiman Maseko | Kaimu Afisa Ununuzi na Ugavi (W) |
| 8. | Samwel Mtafya | Kny; Afisa Mazingira |
| 9. | Colex Mwakyelu | Afisa Mipango (W) |
| 10. | Mwajuma Sekelela | Afisa Mapato |
| 11. | Hawa Mdoka | Mratibu wa TASAF |
| 12. | Loyce Mnyenyelwa | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 13. | Bioto Elisha | Kaimu Mkaguzi wa Ndani (W) |
| 14. | Elias Malinjanga | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W) |
| 15. | Sebastian Kaole | Kny; Mratibu wa UKIMWI |
| 16. | Dkt. Christina Guveti | Mganga Mkuu (W) |
| 17. | Edwin Lupili | Kaimu Mweka Hazina (W) |
| 18. | George Ogutu | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 19. | Chrisantus Kyula | Kny; Afisa TEHAMA |
| 20. | Raphael Mwesongo | Mratibu iCHF |
| 21. | Remigi Lipiki | Kaimu Afisa Ardhi |
| 22. | Kelvin Kalengela | Afisa Biashara |
| 23. | Mhuli Magembe | Afisa Uchaguzi |
| 24. | Ahamad Kiwanga | Kny; Mhandisi Ujenzi (W) |

**SEKRETARIETI**
1. Ferdinand Kaulule
2. Unambwe Afrael

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/27/10/2021 - KUFUNGUA KIKAO**

Katibu aliwakaribisha wajumbe na kuwajulisha kuwa kikao hicho ni cha kawaida kujadili taarifa za utekelezaji robo ya kwanza kwa kipindi cha **Julai-Septemba, 2021** na kumkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuhudhuria na kuwaomba kujadili ajenda zilizowasilishwa. Baada ya maelezo hayo alifungua kikao saa **4:06** asubuhi.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/28/10/2021-KURIDHIA AJENDA**
Ajenda kumi na nane (18) ziliwasilishwa na kuridhiwa kuwa mwongozo wa kikao hicho.

**Ajenda hizo ni;**
1. Kufungua kikao
2. Kuridhia ajenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe **15-09-2021**
4. Yatokanayo na kikao cha tarehe **15/09/2021**
5. Taarifa ya mapato na matumizi mwezi **Septemba, 2021**
6. Taarifa za utekelezaji wa kazi za kawaida za Idara/Vitengo kwa kipindi cha **Julai-Septemba, 2021**
   i. Idara ya Utumishi na Utawala
   ii. Kitengo cha TEHAMA
   iii. Kitengo cha Sheria
   iv. Kitengo cha Ununuzi na Ugavi
7. Taarifa ya miradi ya maendeleo kwa kipindi cha **Julai-Septemba, 2021**
8. Mapendekezo ya Sheria Ndogo na Kanuni za kudumu za Halmashauri
9. Mapendekezo ya utekelezaji wa mradi wa urasimishaji wa makazi msongamano kwa kushirikiana na Benki ya NMB PLC
10. Taarifa ya zoezi la utambuzi wa walengwa wa kaya maskini kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya TASAF kwa vijiji 19 ambavyo haviko kwenye mpango
11. Taarifa ya mkaguzi wa ndani kwa kipindi cha **Julai-Septemba, 2021**
12. Mapendekezo ya vikundi vitakavyopatiwa mikopo
13. Maombi yakutumia nyumba ya Halmashauri iliyopo maeneo ya bomani kuwa makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Kilombero.
14. Maombi ya kuazima majengo ya ofisi na nyumba za watumishi za Halmashauri zilizopo Ifakara
15. Mapokezi ya fedha za UVIKO-19 za miradi ya maendeleo
16. Mashauri ya nidhamu
17. Mengineyo
18. Kufunga kikao

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/29/10/2021-KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 15/09/2021**
Mwenyekiti aliwaongoza wajumbe kupitia muhtasari wa kikao kilichopita ukurasa mmoja baada ya mwingine na kuthibitisha kuwa ulikuwa sahihi hivyo usainiwe kuwa kumbukumbu ya Halmashauri.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/30/10/2021-YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 15/09/2021**

Kamati ilipokea na kujadili yatokanayo na kikao kilichopita kama ifuatavyo;

a. **Andiko kwa ajili ya umaliziaji wa jengo la ghorofa lililoko Ifakara**

Kamati ilielezwa kuwa uandaaji wa andiko hilo kwenda Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa unaendelea. Kamati iliagiza taarifa ya uandaaji wa andiko hilo kuwasilishwa katika kikao kijacho.

**Azimio:** Taarifa ya uandaaji wa andiko kwa ajili ya kupeleka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa iwasilishwe katika kikao kijacho.

b. **Mpango wa matumizi ya nyumba za Halmashauri zilizopo Ifakara**

Kamati iliagiza mpango wa majengo na nyumba za Halmashauri zilizoko Ifakara uwasilishwe katika kikao kijacho.

**Azimio**: Taarifa ya mpango wa matumizi ya nyumba za Halmashauri zilizoko Ifakara uwasilishwe katika kikao kijacho.

c. **Kuhusu upungufu wa watumishi**

Kamati ilitaka kupata ufafanuzi wa mkakati wa Halmashari kuhusu upungufu wa watumishi uliopo. Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri inaendelea kukumbusha kwenye mamlaka zinahusika ikiwa ni pamoja na kuandika barua kwa Katibu Mkuu Utumihsi yenye **Kumb. Na. MDC/CS.20/18/VOL.IV/78** ya tarehe **02/08/2021** kuhusu suala hilo.

d. **Ufuatiliaji wa hati miliki za nyumba na majengo ya Halmashauri yaliyoko Ifakara**

Kamati iliarifiwa kuwa, malipo kwa ajili ya maombi ya hati miliki za nyumba na majengo ya Halmashauri yanaendelea na taarifa ya ufuatiliaji wa hati hizo itawasilishwa kikao kijacho.

**Azimio:** Taarifa ya ufuatiliaji wa hati miliki za nyumba na majengo ya Halmashauri yaliyoko Ifakara iwasilishwe kikao kijacho.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/31/10/2021- TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2021**

Kamati ilipokea taarifa ya mapato na matumizi kama ifuatavyo;

Halmashauri imekisia kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs.34,170, 930,575.30** katika kipindi cha **Julai 2021** hadi **Juni 2022**. Aidha katika mwaka wa fedha **2020/2021** Halmashauri ilibakiwa na kiasi cha Shilingi **152,735, 352.10.** Hivyo makisio ya jumla kwa mwaka wa fedha **2021/2022** pamoja na bakaa ni Shilingi **34,323,666, 109.40.**

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, kamati ilijadili kama ifuatavyo;

**Kuhusu ongezeko la Tshs. 32,000,000.00 katika bajeti ya 2021/2022**

Kamati ilitaka kupata ufafanuzi wa ongezeko la **Tshs. 32,000,000.00** katika makisio ya bajeti kwa mwaka wa fedha **2021/2022.** Ufafanuzi ulitolewa kuwa ongezeko hilo lilitokana

na fedha ambazo awali TAMISEMI hawakuingiza kwenye mfumo wa matumizi baada ya marekebisho ya bajeti kufanyika.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/32/10/2021- TAARIFA ZA IDARA/VITENGO KWA KIPINDI CHA JULAI-SEPTEMBA, 2021**

Kamati ilipokea taarifa za Idara/Vitengo kama ifuatavyo;

i. **Idara ya Utumishi na Utawala**

Idara ya Utumishi na Utawala imetekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushughulikia mashauri ya nidhamu ya watumishi na kushughulikia mafao ya watumishi wanaostaafu, kuacha kazi au kufariki dunia. Jumla ya watumishi **99** wameajiriwa katika Idara mbalimbali kwa mgawanyo ufuatao: Idara ya Elimu Msingi **37,** Elimu Sekondari **19,** Afya **38**, na Utawala **5.**

Hata hivyo, Halmashauri inakabiliwa na upungufu wa watumishi katika Idara zake kutokana na uhamisho, kustaafu na kufariki ambapo ufuatiliaji unaendelea kufanyika ili kupata kibali cha ajira ili kukabiliana na upungufu uliopo.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, kamati ilipokea na kujadili kama ifuatavyo;

a. **Kuhusu mpango wa malipo ya fedha za wastaafu za kusafirisha mizigo**

Kamati ilitaka kupata ufafanuzi wa mpango wa Halmashauri kuhusu malipo ya fedha za kusafirisha mizigo ya wastaafu. Ufafanuzi ulitolewa kuwa, Halmashauri imekuwa ikipunguza madeni ya fedha hizo kwa awamu kadri fedha zinavyopatikana. Hata hivyo, Halmashauri imepokea **Tshs. 36,500,000.00** kutoka serikali kuu kwa ajili ya kuwalipa walimu waliostaafu. Kamati iliagiza taarifa ya wastaafu wanaodai fedha za kusafirishia mizigo iwasilishwe katika kikao kijacho.

**Azimio:** Taarifa ya wastaafu wanaodai fedha za kusafirisha mizigo iwasilishwe katika kikao kijacho.

b. **Kuhusu malipo ya fedha za uhamisho wa watumishi kutoka Ifakara kuja Mngeta**

Kamati ilitaka kupata ufafanuzi wa malipo ya fedha za uhamisho wa watumishi waliohama kutoka Ifakara kuja Mngeta. Ufafanuzi ulitolewa kuwa Halmashauri ilipanga kukamilisha malipo hayo kufikia tarehe 30-06-2021 isipokuwa ilishindwa kumaliza kulipa watumishi wote kutokana kushindwa kufikia lengo la kukusanyo kwa mwaka 2020/2021. Iliongezwa kuwa, watumishi hao hao wanaendelea kulipa kadiri fedha zinavyopatikana. Pamoja na maelezo hayo, kamati iliagiza taarifa ya watumishi ambao hawajamaliza kulipwa fedha za uhamisho kutoka Ifakara kuja Mngeta iwasilishwe katika kikao kijacho.

**Azimio:** Taarifa ya watumishi ambao hawajamaliza kulipwa fedha za uhamisho kutoka Ifakara kuja Mngeta iwasilishwe katika kikao kijacho.

**ii. Kitengo cha Sheria**

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2021 Halmashauri ilikuwa na kesi tatu (3) Mahakamani. Kesi zote ziko kwenye hatua mbalimbali za kusikilizwa. Kati ya kesi hizo tatu, kesi mbili zinahusu migogoro ya ardhi na kesi moja inahusu mkataba wa ujenzi wa barabara ya Chita – Merera ambayo hata hivyo imewasilishwa kwa Wakili Mkuu wa Serikali kwa ajili ya hatua zake.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, kamati ilipokea.

**iii. Kitengo cha Ununuzi na Ugavi**

Halmashauri ilifanya manunuzi mbalimbali kwa idara zake kwa kipindi hiki yenye jumla **Tshs. 142, 627,336.00** kwa kuzingatia sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2013.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, kamati ilipokea.

**iv. Kitengo cha TEHAMA**

Kitengo kimehuisha akaunti 50 za walimu wa sekondari katika mfumo wa usajili wa wanafunzi wa Baraza la Mitihani Tanzania (PREMS), kukagua na kuhuisha toleo jipya la kuongeza ulinzi kwenye mashine 38 za ukusanyaji mapato pamoja na kuongeza mashine nne za kukusanya mapato katika kata ya Mofu, Masagati, Namwawala, na Chisano.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, kamati ilipokea.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/33/10/2021- TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI-SEPTEMBA, 2021**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri imeidhinishiwa kutumia **Tshs. 10,937,092,382.30** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo. Katika kipindi hicho, Halmashauri imepokea **Tshs. 1,484,440,519.78** na kutumia **Tshs. 664,383,984.38.**

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa kamati ilipokea.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/34/10/2021- KUPITISHA SHERIA NDOGO NA KANUNI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI**

Kupitia *Tangazo la Serikali Na. 305A la tarehe 5/5/2020* Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ilianzishwa rasmi ambapo miongoni mwa nyenzo zake muhimu za utawala ni sheria ndogo. Hata hivyo, tangu kutolewa kwa tangazo hilo, Halmashauri imekuwa ikitumia sheria ndogo na Kanuni za Kudumu za iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero katika kipindi cha mpito. Kwa sasa, hususani baada ya Baraza la Madiwani kurejea Halmashauri hainabudi kupitisha sheria ndogo zake.

Hivyo, ridhaa inaombwa ili rasimu za sheria ndogo za Ada na Ushuru, Kodi ya Huduma, Kituo cha Mabasi, Hifadhi ya Mazingira, Madini ya Ujenzi na Kuzuia Upotevu wa Mazao baada ya Mavuno na Usimamizi wa Masoko pamoja na Kanuni za Kudumu za Halmashauri

zinazowasilishwa ziridhiwe na kupitishwa. Aidha, maoni ya Kamati za Maendeleo za Kata yamechambuliwa na kuingizwa kwenye rasimu hizo kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

Kamati ilipokea, ilijadili na kuridhia mapendekezo hayo kwa ajili ya hatua za utekelezaji.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/35/10/2021- MAPENDEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA URASIMISHAJI WA MAKAZI MSONGAMANO KWA KUSHIRIKIANA NA BENKI YA NMB PLC**

Urasimishaji wa makazi msongamano ni mchakato wa kuyafanya makazi msongamano yaliyojengwa holela na kuyafanya kuwa rasmi kisheria, mchakato huu unaambatana na uwekaji wa miundombinu muhimu ya barabara pamoja na njia za miguu ili kufanya kila kiwanja kiweze kufikika. Miongoni mwa faida zitakazopatikana ni pamoja na wananchi kuweza kutumia ardhi zao kama mtaji/dhamana ya kukopesheka kwenye taasisi za kifedha.

Ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika miradi ya urasimishaji, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya NMB wameingia mkataba ambapo Benki imeridhia kuwakopesha wananchi wanaofanyiwa urasimishaji kupitia akaunti zao maalum za urasimishaji. Fedha zitakazotolewa na Benki zitagharamia zoezi la utambuzi wa vipande vya ardhi, uandaaji wa mchoro wa mipangomiji, upimaji wa maeneo husika pamoja na umilikishaji. Wananchi katika eneo husika watawekewa kiasi stahiki kwenye akaunti zao kama mkopo ambao ataurejesha ndani ya miezi 24 kwa riba ya asilimia 10 (10%) kwa mwaka.

Kamati ilipokea na kuridhia taarifa hiyo kwa ajili ya utekelezaji.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/36/10/2021- UTAMBUZI WA WALENGWA WA KAYA MASIKINI KIPINDI CHA PILI CHA AWAMU YA TATU YA TASAF KWA VIJIJI 19 AMBAVYO HAVIKO KWENYE MPANGO**

Utambuzi wa walengwa wa kaya masikini kwa vijiji ambavyo haviko kwenye mpango ulifanyika kuanzia tarehe **6/7/2021** hadi tarehe **26/7/2021**. Vijiji 19 vilishiriki katika zoezi hilo ambavyo ni Idete A, Idete B, Udagaji, Miwangani, Mpofu, Namalumbo, Ngajengwa, Igima, Chiwachiwa, vingine ni Kamwene, Tanganyika, Msolwa, Utengule, Ipugasa, Mpanga, Iduindembo, Ngalimila, Mgugwe na Chisano. Jumla ya wawezeshaji 21 walishiriki katika zoezi hilo na kaya **1,948** ziliibuliwa na kuwasilishwa TASAF makao makuu kwa hatua zaidi. Kamati ilipokea na kuridhia taarifa hiyo kwa utekelezaji.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/37/10/2021-TAARIFA YA HOJA ZA MKAGUZI WA NDANI**

Jumla ya hoja tisa (9) zilitolewa ambazo ni pamoja na leseni za biashara ambazo zimelipiwa kwenye mfumo wa kukusanyia mapato lakini hazikutolewa kwa wateja, kutowasilishwa kwa kodi ya zuio TRA (Non submission of withholiding tax to TRA) **Tshs.50,400.00**, mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ambayo haijarejeshwa **Tshs. 16,919,100.00** na ununuzi wa bidhaa na huduma usioambatana na stakabadhi za mfumo wa kieletroniki zenye jumla ya **Tshs.4,520,000.00.**

Kamati ilipokea na kushauri menejimenti kuongeza nguvu ya ufuatiliaji wa deni la makusanyo ili kuondokana na hoja hiyo.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/38/10/2021- MAPENDEKEZO YA VIKUNDI VILIVYOOMBA MKOPO KUPITIA MFUKO WA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

Kwa mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri inakusudia kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi **618,000,000.00** kwa vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Kiasi cha shilingi **275,000,000.00** ni fedha za asilimia kumi inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri, ambazo zitatolewa kwa vikundi **32** vyenye shughuli za kiuchumi ambapo kiasi cha shilingi **204,000,000** zitatolewa kwa vikundi **24** vya wanawake, kiasi cha shilingi **69,000,000.00** kwa vikundi **07** vya vijana na kiasi cha shilingi **2,000,000.00** kwa kikundi **01** cha watu wenye ulemavu.

Kiasi cha shilingi **343,000,000.00** ni fedha za marejesho ambazo zitatolewa kwa vikundi **30** kati ya hivyo, vikundi **19** vyenye thamani ya shilingi **183,000,000.00** ni vya wanawake, vikundi **10** vyenye thamani ya shilingi **154,000,000.00** ni vya Vijana na kiasi shilingi **6,000,000.00 kimetolewa** kwa mlemavu **01**. Orodha ya wanufaika wa Mkopo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 yenye thamani ya **Sh.618, 000,000.00** kwa kata za Idete, Mchombe, Mngeta, Ching'anda, Chisano, Kamwene, Masagati na Kalengakelu iliwasilishwa.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa, kamati ilipokea kwa ajili ya utekelezaji.

**MUHTASARI NA.MDC/FUM/39/10/2021- MAOMBI YA KUTUMIA NYUMBA YA HALMASHAURI KUWA MAKAZI YA MKUU WA WILAYA YA KILOMBERO**

Halmashauri ilipokea barua yenye Kumb.**Na CAB.2/182/01/28** ya tarehe **23/09/2021** kutoka ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuhusu maombi ya kutumia nyumba ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba iliyopo maeneo ya bomani kuwa makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Kilombero ikirejea barua ya Katibu Tawala Mkoa kwamba Mkoa hauna pingamizi isipokuwa ridhaa inapaswa kutolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba.

Kamati ilipokea na kueleza kuwa, Halmashauri iliweka nyumba na majengo yaliyopo Ifakara kwenye mpango wa bajeti wa Halmashauri kwa ajili ya kukusanya mapato na baadhi ya ofisi na nyumba tayari zina wapangaji. Hivyo, nyumba hiyo ni miongoni mwa nyumba zilizo katika mpango huo.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/40/10/2021- OMBI LA KUAZIMA MAJENGO YA OFISI NA NYUMBA ZA WATUMISHI**

Halmashauri ilipokea barua yenye kumb. **Na.MDC/A.10/3/22** ya tarehe **11/10/2021** kuhusu ombi la kuazima baadhi ya majengo ya ofisi na nyumba za watumishi zilizopo katika Halmashauri ya Mji Ifakara. Nyumba zinazoazimwa ni pamoja na Nyumba iliyokuwa inatumiwa na Mkuu wa Idara ya Utumishi pamoja na Maendeleo ya Jamii, majengo yaliyokuwa yanatumiwa na kitengo cha Maliasili, maendeleo ya Jamii, Kilimo, mifugo na uvuvi, kitengo cha manunuzi pamoja jengo la mgahawa.

Kamati ilipokea ombi hilo na kuelekeza kuwa, tayari Halmashauri imeweka katika mpango wa bajeti kwa ajili ya kukusanya mapato kupitia majengo hayo na tayari baadhi ya ofisi na nyumba zina wapangaji. Hivyo, Halmashauri ipo tayari kutoa nyumba na majengo hayo kwa Halmashauri ya Mji kwa kuwapangisha ili kuendana na malengo yaliyowekwa na Halmashauri katika ukusanyaji wa mapato.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/41/10/2021- MAPOKEZI YA FEDHA ZA UVIKO-19**

Halmashauri imepokea **Tshs. 1,727,719,151.80** kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa **UVIKO – 19.** Kuendesha shughuli za chanjo **Tshs. 47,719,151.80**, Ujenzi wa vyumba **78** vya madarasa na madawati katika shule za Sekondari **Tshs. 1,560,000,000.00,** ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum shule ya msingi Ngajengwa **Tshs. 80,000,000.00**, ujenzi wa vyumba viwili (**2**) vya madarasa shule Shikizi Msesere (Mngeta) **Tshs. 40,000,000.00** na ujenzi wa nyumba ya mtumishi katika Hospitali ya Halmashauri **Tshs. 90,000,000.00**. Fedha hizo zote zimeingizwa kwenye akaunti za shule husika.

Kamati ilipokea na kuridhia taarifa hiyo kwa ajili ya utekelezaji.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/42/10/2021-MENGINEYO**
Hakukua na mengineyo yaliyopokelewa katika kikao hicho.

**MUHTASARI NA. MDC/FUM/43/10/2021-KUFUNGA KIKAO**
Baada ya ajenda zote kujadiliwa, katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao. Kabla ya kufunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na kusisitiza kuwa maagizo na maelekezo yaliyotolewa yafanyiwe kazi. Baada ya maelezo hayo alifunga kikao saa **2:13** Usiku

Eng. S.B. Kalinga ........................................ | UMETHIBITISHWA
KATIBU | HON. INNOCENT S. MWANGALA ........................................
| MWENYEKITI
........................................ | ........................................
SAHIHI | SAHIHI

**TAREHE**...23/11/21...

## YATOKANAYO NA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO CHA TAREHE 25/10/2021

| MUHTASARI NA. | AZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| **MDC/FUM/30/10/2021** | Taarifa ya uandaaji wa andiko kwa ajili ya kupeleka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa iwasilishwe kikao kijacho. | **DPLO** | Andiko limeandikwa, hatua iliyofikia sasa ni kuandaa BOQ na kukokotoa hesabu za namna ya kulipa deni hilo na kufanya hesabu za uchambuzi wa kiuchumi (Economical Analysis) kama tulivyoshauriwa na wenzetu waliokwishapata mikopo toka bodi hiyo. |
| **MDC/FUM/32/10/2021** | Taarifa ya mpango wa matumizi ya nyumba zilizoko Ifakara iwasilishwe kikao kijacho. | | Azimio limetekelezwa, angalia kiambatisho. |
| | Taarifa ya wastaafu wanaodai fedha za kusafirisha mizigo iwasilishwe kikao kijacho. | **DHRO** | Azimio limetekelezwa, angalia kiambatisho. |
| | Taarifa ya ufuatiliaji wa hati miliki za nyumba na majengo ya Halmashauri iwasilishwe kikao kijacho | **DLO** | Azimio limezingatiwa, malipo yamefanyika kwenye akaunti ya Wizara. Kinachosubiliwa ni kukamilika kwa rasimu ya hati zinazoandaliwa na Halmashauri ya Mji Ifakara. |
| | Orodha ya watumishi ambao hawajamaliza kulipwa fedha za uhamisho kutoka Ifakara kuja Mngeta iwasilishwe katika kikao kijacho. | **DHRO** | Kiasi cha **Tshs. 662,874,600.00** kilikuwa kinadaiwa kulipa watumishi waliohamia Mngeta kutoka Ifakara. Hadi kufikia Novemba 19, 2021, kiaisi cha **Tshs. 467,572,800.00** zimelipwa na kubakia **Tshs. 195,301,800.00** orodha ya watumishi ambao bado wanadai itawasilishwa kwenye kikao. |